*Kioo cha Lugha, Juz. 21(1), 151-168*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v21i1.9

# Tafsiri ya Lugha ya Ishara katika *Wema Hawajazaliwa*: Mtazamo wa Ulinganifu wa Kimawasiliano

*Birigitha N. John*[1]

## Ikisiri

Tafsiri ni taaluma kongwe ambayo imekuwa ikifanyika katika nyuga mbalimbali kama vile sheria, utabibu na lugha. Tafiti nyingi zimekitwa katika matatizo ya tafsiri kwa ujumla. Wataalamu wa tafsiri, hususani za kifasihi kama vile Mkinga (2005), Malangwa (2010) na Mekacha (2013), wametafiti kuhusu mbinu na matatizo ya kutafsiri matini za kifasihi. Data za makala hii zimetokana na mbinu ya uchambuzi wa matini na usaili. Wafasiri tofauti wametafsiri kazi za kifasihi kwa kuzingatia usanaa uliomo kwenye kazi husika. Makala hii inamulika tafsiri ya lugha ya ishara katika *Wema Hawajazaliwa* kwa kuzingatia mtazamo wa ulinganifu wa kimawasiliano. *Wema Hawajazaliwa* ni riwaya iliyotafsiriwa na Abdilatif Abdallah kutoka katika riwaya ya *The Beautyful Ones are not Yet Born* ya Ayi Kwei Armah. Makala hii iliongozwa na Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano iliyoasisiwa na Nida (1964). Pamoja na wataalamu wengi kutafiti kuhusu matatizo ya tafsiri, bado tafsiri ya kifasihi haijafanyiwa tafiti za kutosha hususani katika lugha ya Kiswahili. Makala hii imebaini kuwa, mfasiri huzingatia lugha ya ishara katika tafsiri ya matukio mbalimbali ya kiishara.

## 1.0 Utangulizi

Makala hii imemakinikia tafsiri ya lugha ya ishara kwa kuchunguza matukio ya kiishara katika riwaya ya *Wema Hawajazaliwa*. Malangwa (2005) anasema kuwa kazi ya kutafsiri matini za kifasihi ni ngumu, kwa sababu inakumbana na changamoto mbalimbali kama vile tofauti baina ya lugha chanzi (LC) na lugha lengwa (LL). Mfasiri wa matini za kifasihi ana jukumu kubwa la kuhakikisha matini anayoifanyia tafsiri inadumisha umbo la kifasihi, kwa kujiegemeza katika pande kuu muhimu za fasihi ambazo ni fani na maudhui. Kwa upande wa fani, matumizi ya lugha ni kipengele kimojawapo ambacho kina umuhimu mkubwa katika kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Hivyo, mfasiri anapaswa kuelewa vyema kipengele hiki kinachohusisha mambo mbalimbali, kama vile

[1] Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania. Baruapepe: birigithangwano@gmail.com

matumizi ya lugha ya ishara, ambayo hufanya kazi nyingi katika kazi za kifasihi, kwa mfano, kuifanya kazi iwe na mvuto wa kipekee kwa msomaji, kuwasilisha dhamira, ujumbe na kuonesha weledi wa kisanaa wa mtunzi. Wanyonyi (2015) anasisitiza kuwa, lugha ya ishara hutumika kama mbinu ya mtindo ambayo huwa nyenzo ya kuwasilisha maana katika matini za kifasihi, ambapo ishara huweza kuwa na maana zaidi ya moja. Katika muktadha wa kifasihi, lugha ya ishara hutumiwa kumaanisha lugha wanayotumia watu, vitu, mahali, jambo, hali au tukio kuwakilisha maana tofauti na ile inayoelezewa kwa namna ya uficho. Makala hii inajadili tafsiri ya lugha ya ishara katika riwaya ya *Wema Hawajazaliwa* kwa kuzingatia mtazamo wa ulinganifu wa kimawasiliano.

## 2.0 Muhtasari wa Riwaya ya *Wema Hawajazaliwa*

*Wema Hawajazaliwa* (1976) ni riwaya iliyotafsiriwa kwa Kiswahili na Abdilatif Abdallah kutoka katika riwaya ya *The Beautyful Ones are Not Yet Born* (1968) ya Ayi Kwei Armah kwa lugha ya Kiingereza. Riwaya hii inazungumzia nchi ya Ghana kwa kuonesha namna utoaji wa rushwa ulivyokithiri katika nchi hiyo. Hadithi inamhusu mhusika mkuu anayejulikana kwa jina la Yule Bwana ambaye ingawa ni mtu asiyependa rushwa, anaishi katika jamii inayopalilia rushwa. Hali hii inasababisha mgogoro wa kifamilia kati ya Yule Bwana na mkewe Oyo. Yule Bwana anaonekana kuwasaidia wala rushwa pasipo kuonesha jitihada zozote za kudhibiti rushwa. Kwa mfano, tunamwona Yule Bwana akimsaidia kumtorosha Koomson ambaye alikuwa waziri katika serikali ya Nkurumah ambayo haifanyi vizuri katika uongozi wake. Viongozi wa jeshi wanaamua kufanya mapinduzi ya kijeshi ili kuigeuza serikali iliyopo madarakani. Hata hivyo, hakukuwa na mabadiliko yoyote yanayozalishwa kwa sababu rushwa bado iliendelea kukithiri.

## 3.0 Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano

Nadharia ya ulinganifu wa kimawasiliano ipo katika kundi la nadharia za ulinganifu. Nadharia zingine katika kundi hili ni Nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo na Nadharia ya Ulinganifu wa Aina za Matini. Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano iliasisiwa na Nida (1964) na baadaye iliendelezwa na waasisi wengine ambao ni Catford (1965), Nida na Taber (1969) na Reiss (1971 na 2000). Nida (1964) aliitumia Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano kuanzia miaka ya 1960 wakati alipokuwa akifanya tafsiri za Biblia (Pembe, 2016). Jilala (2016) anasema kuwa Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano ni mkabala unaosisitiza ulinganifu katika ujumbe na mtindo baina ya lugha chanzi (LC) na lugha Lengwa (LL).

Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano ni ya kwanza ya tafsiri ya kimawasiliano ambayo inalenga kuondoa tofauti zilizomo baina ya utamaduni na isimu katika tafsiri. Nadharia hii imeleta mapinduzi katika tafsiri na kuifanya tafsiri

kuwa kazi ya kisayansi. Jambo muhimu linalosisitizwa na nadharia hii ni kuleta athari sawa kwa hadhira ya matini lengwa kama ilivyo kwa hadhira ya matini chanzi. Makaryk (1993) anasisitiza kuwa ili tafsiri iwe na ulinganifu wa kidhima ni lazima isionekane kuwa tafsiri, bali kazi asilia katika lugha lengwa. Kwa hivyo, anasisitiza kwamba mfasiri anapaswa kutafuta visawe linganifu katika LL ambavyo vinalingana kidhima na vya LC.

Nadharia hii ina mihimili mitatu mikuu ambayo ni mosi, usomaji na uelewekaji; mhimili huu unasisitiza kuwa matini chanzi lazima izingatie usomekaji kwa maana ya kusikika vema kwa wasomaji na kuwasilisha taarifa au maudhui pamoja na mtindo. Pili, uasilia na ufafanuzi ambayo ina maana kuwa matini iliyotafsiriwa inatakiwa isomeke kana kwamba imeandikwa katika lugha lengwa. Tatu, uzingatizi wa athari sawa ambao unahusisha wasomaji wa matini lengwa kupata athari sawa kama ilivyo kwa wasomaji wa matini chanzi.

## 4.0 Methodolojia ya Utafiti

Makala hii imetokana na utafiti wa kitaamuli uliohusisha mbinu mbili za ukusanyaji wa data ambazo ni uchambuzi wa matini na usaili. Mkabala wa kitaamuli hutumia zaidi tafakuri katika kuhusisha taarifa mbalimbali za kitafiti na kuhitaji maoni ya kina ya watoataarifa kwa kutumia mbinu ya maelezo (Ponera, 2019). Katika uchambuzi wa matini, kumefanyika usomaji wa kina wa matini chanzi na matini lengwa. Riwaya ya *Wema Hawajazaliwa* ambayo ni matini chanzi imeteuliwa kutokana na kuwa na matumizi ya lugha ya ishara yaliyobainika kupitia utafiti jaribizi. Halikadhalika, vyanzo vingine vya maarifa kama vile makala na tasnifu vimesomwa.

## 5.0 Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano Inavyosawiriwa katika Tafsiri ya Lugha ya Ishara katika *Wema Hawajazaliwa*

Wafasiri wa matini za kifasihi kwa kiasi kikubwa huzingatia misingi ya Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano katika kazi ya kutafsiri. Makala hii imebaini kuwa lugha ya ishara ambayo ni sehemu ya matumizi ya fani imesawiriwa katika riwaya ya *Wema Hawajazaliwa*. Lugha hii ya ishara imejibainisha kupitia wahusika wa kiishara, matukio ya kiishara na kichwa cha riwaya. Aya zifuatazo zinafananua vipengele hivyo:

### 5.1 Matumizi ya Wahusika wa Kiishara

Wahusika ni watu, wanyama au viumbe ambao hutumika katika kazi ya fasihi (Samweli, 2015). Aidha, waandishi hutumia baadhi ya wahusika wa kiishara kwa ajili ya kuwasilisha maana ya ziada kupitia uhusika wao. Wafasiri wa kazi za fasihi wana jukumu la kutafsiri wahusika na uhusika wao katika kazi husika. Wamitila (2008) anaeleza kuwa, wahusika ndio watendaji wakuu katika kazi za fasihi.

Watunzi wa kazi za kifasihi hutumia wahusika katika kufikisha ujumbe wao kwa hadhira waliyoikusudia. Wakati mwingine, watunzi hawa hutumia wahusika wa kiishara katika kuwapa maana fulani ya kificho ambayo wasomaji wanapaswa waing'amue ili kuielewa zaidi. Wafasiri wa matini za kifasihi nao hutafsiri matini hizo kwa namna inayodumisha usanaa wa kifasihi ndani yake ikiwa ni pamoja na kuwatafsiri wahusika hawa na uhusika wao kwa namna inayoleta maana ya kiishara kwa wasomaji wa matini lengwa (Thomas, 2018). Katika utafiti uliofanyika, wahusika waliotafitiwa ni wale ambao uumbaji wao umehusisha matumizi ya lugha ya ishara. Katika *Wema Hawajazaliwa*, kuna wahusika wa kiishara waliojitokeza katika tafsiri ambao ni Yule Bwana na Princess.

Mhusika wa kwanza ni Yule bwana. Huyu ni mhusika mkuu wa riwaya hii. Mhusika huyu ambaye kwenye matini chanzi ameitwa "the man", ametafsiriwa kwa kutumia lugha ya ishara, na ameitwa "Yule bwana". Kwa mujibu wa BAKITA (2015), neno "bwana" ni jina la mwanamume yeyote, aghalabu mtu mzima. Hili linatumika kama jina la jumla ilhali kila mwanamume huwa na jina lake mahususi. Utafiti uliofanyika umebaini kuwa mhusika huyu anayeitwa "Yule Bwana" hajapewa jina mahususi kwa kuwa ni mhusika wa kiishara anayewakilisha watu wengi katika jamii wenye hulka yake. Kilatu (2021)[2] anasema kuwa mhusika huyu amepewa jina la "Yule Bwana" kuwakilisha watu wa kawaida wasio na hadhi katika jamii. Hivyo, tunaweza kusema kuwa, Yule Bwana anasimama badala ya watu wa tabaka la chini, yaani watu maskini. Kwa mfano, tunaona Yule Bwana akiwa na choo duni kiasi cha kujizuia haja mpaka afike kwenye vyoo vya ofisini. Hii inadhihirika kupitia jozi ifuatayo:

**Jozi Na. 1**

**LC**: *But the rumble subsided, and he knew he could wait till he got to the office* (pg. 101).

**LL**: Lakini mara kule kuunguruma kukatulia, na akawa na yakini kwamba ataweza kujizuia mpaka afike ofisini (uk. 109).

Katika data iliyowasilishwa kwenye Jozi Na. 1, tunaona Yule Bwana anavyosawiri hali ya umaskini na kuwakilisha watu wa tabaka la chini. Watu hawa ni wengi katika jamii ya Ghana ambayo inaongozwa na viongozi wasio waadilifu kama vile akina Koomson.

[2] Emmanuel Kilatu ni Mhadhiri wa Fasihi ya Kiingereza katika Idara ya Fasihi na Lugha za Kigeni, Chuo Kikuu cha Dodoma. Alimsailiwa kwa njia ya simu tarehe 15/05/2021.

Mhimili wa Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano unaosisitiza kuwa tafsiri inatakiwa isomeke na kueleweka vyema kwa wasomaji, umezingatiwa. Hii imejitokeza ambapo mfasiri ametafsiri kuhusu mhusika na uhusika wa "Yule Bwana" aliyebeba lugha ya ishara kwa namna inayosomeka na kueleweka vema. Mhusika huyu hajapewa jina kwa sababu anaonekana kuwa ni mhusika aliyekosa utambulisho kamili wa kuwa yeye ni nani. Kuna wakati, anakataa rushwa ikiwa na maana kwamba yuko upande wa wapenda mema; lakini, kuna wakati anawasaidia watenda maovu kama alivyosaidia kumtorosha Koomson ambaye ni kiongozi asiye mwadilifu na mla rushwa. Utafiti umebaini kuwa kitendo cha Yule Bwana kusaidia kumtorosha Koomson kimebeba lugha ya ishara inayoonesha unafiki wa baadhi ya watu katika jamii. Unafiki huo unabainika kwa mhusika Yule Bwana anayeichukia rushwa lakini yuko tayari kushirikiana na wala rushwa.

Mhusika wa pili ni Princess. Huyu ni mtoto wa Joseph Koomson anayependwa sana na baba yake kuliko watoto wengine. Uishara wa mhusika huyu unajitokeza pale ambapo Yule Bwana na mkewe, Oyo, wanaenda kuwatembelea. Yule Bwana anamuulizia na kujibiwa kama ifuatavyo:

**Jozi Na. 2**

**LC**: *I didn't know your first born had become such a young lady. What is her name? 'Princess,' said Estella. 'Is that her real name, or some sort of nickname?' Asked the man. 'It's her name,' said Estella* (pg. 148).

**LL**: Sikujua kwamba mtoto wako wa kwanza ameshavuta kimo vile. Anaitwaje? Princess, akajibu Estella. "Hilo ndilo jina lake hasa au ni la lakabu tu?" Yule Bwana akauliza, "Ndilo lake hasa" akasema Estella (kur. 161-162).

Katika Data ya Jozi Na. 2, tunaona Yule Bwana anashangaa mtoto wa Koomson kuitwa Princess, jina la Kiingereza. Princess ni jina lenye maana ya mtoto wa kike wa mfalme au chifu. Kitendo cha Koomson kumwita mtoto wake Princess kinaashiria ukoloni mamboleo kwa Waafrika, yaani kutukuza utamaduni wa Kizungu na kutothamini utamaduni wa Kiafrika. Duwe (2021)[3] anashadidia hoja hii kwa kusema:

> Sisi Waafrika tuna utaratibu wetu wa kuwaita watoto majina. Miongoni mwa utamaduni huo ni pamoja na kuzingatia kipindi au tukio ambalo

[3] Martina Duwe ni Mhadhiri Msaidizi wa taaluma za Kiswahili katika Chuo Kikuu Mzumbe. Pia, ni mwanafunzi wa shahada ya uzamivu katika Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma. Alimsaili na mtafiti tarehe 20/04/2021 katika viunga vya Chuo Kikuu cha Dodoma.

> lilitokea mtoto anapozaliwa. Kwa mfano, jamii za Wasukuma huita watoto majina kama vile Kabula na Mabula kuashiria kuwa walizaliwa kipindi cha mvua. Pili, Waafrika hupenda kuwapa watoto majina ya kurithi, yaani kama majina ya ndugu zake mfano babu, bibi, na shangazi. Tatu, Waafrika huwapa watoto wao majina ya watu maarufu katika jamii yao. Mbali na kuona baadhi ya taratibu za kuwapa watoto majina katika jamii ya Kiafrika, kwa hivi sasa kutokana na kukua kwa utandawazi ambao unaenda sambamba na ukoloni mamboleo, Waafrika wengi huwapa watoto wao majina ya Kizungu na huona fahari kufanya hivyo pasipo kujua kuwa wanadidimiza utamaduni wao.

Hapa, tunaona Koomson naye ameingia kwenye kundi kubwa la watu waliogubikwa na fikra za ukoloni mamboleo kwa kusifia na kupenda kuwaita watoto wao majina ya Kizungu badala ya majina ya Kiafrika. Katika riwaya teule, tunawaona wahusika wengine kama vile mtoto wa Yule Bwana anayeitwa Deede ambalo ni jina la Kiafrika.

Fauka ya hayo, kutokana na kuvutiwa na jina hilo la mtoto wake, Princess, Koomson anaita mashua yake jina hilo. Hii inaonekana pale ambapo mwandishi anaeleza:

**Jozi Na. 3**

**LC**: *Occasionally, when on a breezy day he happened to wander in the direction of the fishing harbor, he saw it lying there upon the blue-green water of the sea, with the name of Koomson’s little daughter lettered neatly in front of it: PRINCESS* (pg. 152).

**LL**: Siku mojawapo alipopata nafasi kwenda kutembeatembea upande wa forodhani ili kupunga upepo, aliiona hiyo mashua ikielea. Jina la mtoto wa Koomson lilikuwa limechorwa vizuri upande wa mbele wa hiyo mashua: PRINCESS (uk. 165).

Kitendo cha mashua hiyo kuitwa Princess kinadhihirisha wazi kuwa Koomson anampenda mtoto wake na analipenda jina hilo. Ingekuwa halipendi, angeweza kuiita jina lingine lolote la Kiafrika. Suala hili bado linaendeleza kuashiria ukoloni mamboleo uliopo katika jamii za Kiafrika.

Aidha, utafiti umebaini kuwa, mhusika Princess ambaye ametumika kiishara anasawiri namna ambavyo Waafrika hawathamini utamaduni wao. Hii inaonesha kuwa Waafrika, mara nyingi, hawathamini vitu vyao; badala yake, wanapenda kuutukuza utamaduni wa kigeni. Wapo baadhi ya Waafrika wanaothamini majina ya Kiafrika. Mathalani, kwa jamii ya Waswahili, chambilecho Samwel (2015), kuna baadhi ya Waswahili ambao huita watoto wao majina yenye maana fulani kwa

kuangazia tukio au jambo linaloigusa jamii. Kwa mfano, jina la Mwamvita lina maana ya mtoto aliyezaliwa wakati wa vita na Mwanjala ni mtoto aliyezaliwa wakati wa njaa kali. Hii inaonesha kuwa kuna baadhi ya watu wanaotoa majina kwa kufuata Uafrika. Legere (2009) anashadidia kwa kusema kuwa, majina ya Kitanzania huwa na asili yake, lakini cha kushangaza ni kwamba Waafrika wengi hupendelea kuwaita watoto wao majina yenye asili ya nje ya Afrika. Hali hii inasababishwa na watu hao kutothamini utamaduni wao.

### 5.2 Matumizi ya Matukio ya Kiishara

Kipengele cha pili ambacho kinadhihirisha tafsiri ya lugha ya ishara ni matumizi ya matukio ya kiishara. Haya ni matukio yaliyobeba lugha ya ishara ambayo huandikwa kwa namna inayoleta aina mbili za maana, yaani maana msingi na maana ya kiishara (Kahigi, 1995). Maana msingi ni ile maana ya wazi inayopatikana katika tukio husika. Maana ya kiishara ni maana fiche inayopatikana katika tukio husika. Kazi za kifasihi hubeba visa na matukio mbalimbali. Kuna wakati, matukio hayo husanwa kwa namna ya kutumia lugha ya ishara ambayo, kutokana na uelewekaji wake, wasomaji huweza kung’amua maana hizo za kiishara zilizokitwa katika matukio hayo. Katika riwaya ya *Wema Hawajazaliwa*, matukio ya kiishara yanayotokana na tafsiri ya matini chanzi ni haya yafuatayo:

Tukio la kwanza ni la Amankwa kumtafuta karani wa nafasi za magari. Anasema kuwa:

**Jozi Na. 4**

**LC**: *And I will make you know that you have really helped me* (pg. 28).

**LL**: Na nitakufanyia la kukuonesha kuwa umenisaidia (uk. 30).

Tukio hili limetumia lugha ya ishara, kwani hapa, tunaona jinsi Amankwa alipofika ofisini na kukutana na Yule bwana na kuanza kumuulizia karani wa nafasi za magari ili aweze kupata nafasi ya kusafirisha magogo yake. Yule Bwana anamweleza Amankwa kuwa karani wa nafasi za magari hayupo ofisini; hivyo, aje wakati mwingine akiwapo ambapo Amankwa ataweza kuomba msaada. Kupitia tukio hili, kuwapo kwa matumizi ya kifungu cha maneno haya “na nitakufanyia la kukuonesha kuwa umenisaidia” ambacho kinabeba lugha ya ishara inayowakilisha rushwa yanadhihirisha kwamba Amankwa alitengeneza mazingira ya kumlaghai Yule Bwana ili amsaidie kusafirisha magogo yake yaliyoko msituni. Pia, tunaona Amankwa akiendelea kumsihi Yule Bwana amsaidie kwa kumwambia:

**Jozi Na. 5**

**LC**: *I am not a child, my friend. If you work in the same office you can eat from the same bowl* (pg. 29).

**LL:** Mimi si mtoto mdogo, rafiki yangu. Ikiwa mnafanya kazi ofisi moja mnaweza kula sahani moja (uk. 31).

Kifungu cha maneno "*If you work in the same office you can eat from the same bowl*" kimetafsiriwa kuwa "Ikiwa mnafanya kazi ofisi moja mnaweza kula sahani moja". Tafsiri hii inaonesha lugha ya ishara ambayo Amankwa anaielekeza kwa Yule Bwana kumaanisha kuwa nchini Ghana, suala la rushwa ni la kawaida na limekuwa likifanyika katika ofisi nyingi. Ndiyo maana anamwambia kuwa yeye si mtoto mdogo kiasi kwamba asielewe watu wanaofanya kazi ofisi moja huwa na tabia zinazofanana. Amankwa, kwa kuona kuwa maneno pekee hayatoshi, anaamua kumpa Yule Bwana fedha ili aweze kumsaidia kupata nafasi ya kusafirisha magogo yake. Yule Bwana anakataa fedha anazopewa na Amankwa na kumwambia hawezi kuzipokea. Yule B, baada ya kufika nyumbani kwake, anamsimulia mke wake jambo hilo kwa kumwambia:

**Jozi Na. 6**

**LC**: *Somebody offered me a bribe today,' he says after a while. 'Mmmmmmm!'One of those timber contractors.' Mmmmm. To do what? To get him an allocation. 'And like an Onward Christian Soldier you refused*?' (pg. 43).

**LL**: Kuna mtu amenipa rushwa leo. Mmmmm, Umfanyie nini? Kumpatia nafasi ya gari 'Na wewe kama Askari wa Kikristo anayesonga mbele, ukaikataa?' (uk. 45).

Data ya Jozi Na. 6 inaonesha Yule Bwana akimsimulia mkewe kilichotokea ofisini. Yule Bwana anaeleza namna alivyokataa kupokea rushwa kutoka kwa Amankwa. Mke wake, baada ya kusikia hivyo, anamkasirikia na kumwita mumewe askari wa Kikristo. Kupitia Data ya Jozi Na. 6, tunaona tafsiri imefanywa kwa namna inayomfanya msomaji wa matini lengwa kupata mawazo yanayoleta athari zenye ulinganifu kama anavyopata msomaji wa matini chanzi. Tukio la Amankwa kutoa rushwa kwa Yule Bwana linaashiria kuwa kitendo cha rushwa kimekuwa jambo la kawaida sana nchini Ghana na mtu ambaye anakataa kupokea rushwa anaonekana kama mshamba au mtu aliyepitwa na wakati.

Tukio la pili ni la Estella kutohitaji kununuliwa mikate. Tukio hilo limeonekana pale linapotafsiriwa kuwa:

**Jozi Na. 7**

**LC**: *Inside the big car the pointed female voice springs and coils around, complaining of fridges too full to contain anything more and of too much bread already bought* (pg. 37).

**LL**: Ndani ya gari hilo kubwa sauti nyembamba ya mwanamke inajitokeza ikilalamika kwamba jirafu zimejaa hazina nafasi ya kuingia kitu chochote kingine na kwamba kumeshanunuliwa mikate ya kutosha (uk. 38).

Katika Data ya Jozi Na. 7, tunawaona akinamama waliokuwa wakiuza mikate wakijaribu kumshawishi Koomson ambaye ni mume wa Estella anunue mikate. Estella alijibu kwa madaha kuwa jirafu zimejaa hazina nafasi ya kuingia kitu chochote kingine. Utafiti umebaini kuwa hali hii inaashiria matabaka katika jamii. Estella na mume wake, Koomson, wanaonekana kuwa watu wa tabaka la juu kwa kuwa wamefanikiwa kuwa na vitu vingi nyumbani kwao. Kwa upande mwingine, kuna tabaka la chini, yaani tabaka la walalahoi wanaotafuta fedha ya kumudu maisha yao kwa kuuza mikate barabarani.

Tukio la tatu ni la Estella kutokubali kupeana mikono na Yule Bwana. Tukio hili limebeba lugha ya ishara. Mwandishi anaeleza:

**Jozi Na. 8**

**LC:** *The woman's wire voice changes a little in tone. 'Aaaa, ei look. I didn't see anybody.' Out through the window she holds out a hand and something glitters in the night light. The man takes the hand. Moist like lubricated flesh. It is withdrawn as quickly as if contact was a well calamity, and the woman inside seems plainly to have forgotten about the man outside* (pg. 38).

**LL:** Sauti ya ukali ya mwanamke ikabadilika kidogo. "Aaaa, eti tazama. Sikuwa nimekuona". Anatoa mkono wake kupitia dirishani na kuna kitu kinameremeta. Yule Bwana anaupokea mkono kama nyama iliyopakwa mafuta. Unarudishwa ndani upesi kama kwamba huko kuamkiana kulikuwa ni msiba mkubwa unaojulikana sana na mwanamke aliyeko ndani anaonyesha kama ambaye amesahau habari ya mtu aliye nje (kur. 39 - 40).

Kupitia Data ya Jozi Na. 8, tunaona Estella anakataa kupeana mkono na Yule bwana. Kitendo hiki kinaleta maana ya kuwa Estella anadharau na anajiona kuwa yupo daraja la juu kiasi kwamba hawezi kuchangamana na watu masikini au watu wa

tabaka la chini. Tukio linalofanana na hili linajitokeza wakati Estella na Koomson wanakwenda kumtembelea Yule Bwana:

**Jozi Na. 9**

**LC**: *Estella Koomson's handshake was limp, and she withdrew her hand in an insulting hurry* (pg. 130).

**LL**: Yule Bwana alipopeana mkono na Estella, Estella akaurudisha haraka (uk. 141).

Katika Data ya Jozi Na. 9, tunaona namna Estella anavyourejesha haraka mkono wake ili asiweze kupeana na Yule Bwana. Tukio hili bado linaashiria suala la udhalilishaji, yaani, watu wenye uwezo wanaona wasio na uwezo kama takataka na wasiokuwa na maana yoyote. Tukio la Estella kukataa kupeana mkono na Yule Bwana ni ishara ambayo ina viashiria vingine kama vile matabaka katika jamii na kuweka msisitizo kuwa daima watu wa tabaka la juu ni vigumu kuchangamana na watu wa tabaka la chini kama ilivyokuwa kwa Estella ambaye ni mtu wa tabaka la juu na Yule Bwana ni mtu wa tabaka la chini.

### 5.3 Matumizi ya Jina la Riwaya

Kipengele cha tatu ambacho kinadhihirisha tafsiri ya lugha ya ishara ni matumizi ya jina la riwaya. Majina ya riwaya hizi zilizotafsiriwa yametumia lugha ya ishara. Katika *Wema Hawajazaliwa*, jina la riwaya limetafsiriwa kutoka kwenye matini chanzi linalosomeka *The Beautyful Ones Are Not Yet Born*. Jina hili la riwaya limetumia lugha ya ishara yenye kuashiria mambo mbalimbali kama ifuatavyo:

Mosi, katika tafsiri ya jina la riwaya, neno 'wema' limetumika kwa ishara ambayo inawakilisha viongozi wazuri, yaani wanaowajibika katika nafasi zao za uongozi. Jina linaposomeka *Wema Hawajazaliwa* lina maana kuwa viongozi wazuri nchini Ghana bado hawajazaliwa. Kwa muktadha wa riwaya, tunaona kuwa viongozi kama vile Joseph Koomson ni wala rushwa, na si wawajibikaji kwa ujumla. Viongozi wa namna hii wanachangia katika kudidimiza maendeleo ya nchi.

Pili, neno 'hawajazaliwa' katika jina la riwaya limetumika kuashiria ukosefu wa matumaini kwa wananchi juu ya viongozi wa Kiafrika. Hii inaonesha kuwa Afrika bado hakuna viongozi wazuri ambao ni wawajibikaji katika nyadhifa zao. Ukosefu huu wa matumaini unadhihirika katika riwaya katika sura ya 15 kama ifuatavyo:

**Jozi Na. 10**

**LC**: *Behind it, the green paint was brightened with an inscription carefully lettered to form an oval shape:*
*THE BEAUTYFUL ONES*
*ARE NOT YET BORN in the center of the oval was a single flower, solitary, unexplainable, and very beautiful* (pg. 183).

**LL**: Nyuma ya basi hilo, hiyo rangi ya kijani ilizidi kung'arishwa na maneno yaliyochorwa vizuri na yaliyofanya mviringo wa umbo la yai.
WEMA
HAWAJAZALIWA
Katikati ya mviringo huo kulichorwa ua moja lililo zuri lakini lisiloelezeka (uk. 198).

Utafiti umebaini kuwa, gari hili jipya ambalo nyuma limeandikwa "wema hawajazaliwa" linaonesha kukata tamaa kwa wananchi wa Ghana. Hii inaonekana kuwa, hata baada ya mapinduzi ya kijeshi, bado viongozi ni walewale; hakuna mabadiliko makubwa.

Tatu, jina la riwaya la *Wema Hawajazaliwa* linawiana na maneno yaliyokwishakutangulia katika riwaya kuwa hakuna mabadiliko ya tabia za viongozi. Hii inaonekana pale inapoandikwa katika jozi inayofuata:

**Jozi Na. 11**

**LC**: *New people, new style, old dance* (pg. 157).

**LL**: Watu wapya, mtindo mpya, ngoma ya zamani (uk. 171).

Kifungu cha maneno "watu wapya, mtindo mpya, ngoma ya zamani" kinaeleza ukweli kuwa viongozi wazuri katika nchi nyingi za Kiafrika bado hawajazaliwa. Jambo linaloashiriwa hapa ni kuwa ukoloni mamboleo ni kitu kinachotishia ustawi wa utawala bora na maendeleo yakinifu kwa nchi za Kiafrika. Hata kama tunabadilisha viongozi, bado wanabaki kuwa na tabia zinazofanana na za viongozi wa enzi za ukoloni. Said (1977) anashadidia kuwa uhuru wa nchi za Kiafrika si uhuru kamili kwa sababu tumekuwa tukitegemea misaada kutoka kwa nchi zilizoendelea ambazo ndizo zilizotutawala miaka iliyopita. Aghalabu, nchi hizi tegemezi hupewa masharti magumu ili ziweze kupatiwa misaada. Mfano wa masharti hayo ni kukubali kuhalalisha ndoa za jinsi moja.

**5.4 Matumizi ya Mandhari ya Kiishara**

Kipengele cha nne kinachodhihirisha tafsiri ya lugha ya ishara ni matumizi ya mandhari. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), mandhari ni mahali ambapo kazi ya fasihi inatendeka. Kuna aina kuu mbili za mandhari; mandhari halisi na mandhari dhahania. Utafiti uliofanyika umebaini kuwa mandhari ni kipengele kimojawapo ambacho katika tafsiri kimebeba lugha ya ishara. Katika riwaya ya *Wema Hawajazaliwa*, lugha hii ya kiishara inadhihirika kupitia mandhari ya Atlantic – Caprice, mandhari ya choo cha nyumbani kwa Yule Bwana, mandhari ya choo cha ofisini kwa Yule Bwana, mandhari ya mtaa wa makao ya juu na mandhari ya nyumba ya msimamizi wa mashua. Aya zifuatazo zinafafanua mandhari hizo:

Mandhari ya kwanza ni Atlantic – Caprice. Atlantic – Caprice ni jina la hoteli ambalo limetafsiriwa kwa kuachwa jinsi lilivyo kutoka katika MC. Hii ni hoteli kubwa na maarufu ambayo imekuwa ikitembelewa na watu wenye wadhifa kama vile Koomson na mke wake Estella. Kwa mfano, tunaona ikitamkwa pale Koomson anaposema:

**Jozi Na. 12**

**LC:** *Oh, by the way, we are not going back. Atlantic – Caprice and we are late* (pg. 38).

**LL:** Oh, kweli, haturudi nyumbani. Tunakwenda hoteli ya Atlantic – Caprice, na tumechelewa (uk. 40).

Data ya Jozi Na. 12 inaonesha Koomson alikutana na Yule Bwana barabarani na kisha alimwambia kuwa wanakwenda katika hoteli ya Atlantic - Caprice. Katika sehemu nyingine, tunaona baada ya kurudi nyumbani, Yule Bwana anamhadithia mkewe kuwa alikutana na Koomson na mke wake wakienda Atlantic – Caprice. Yule Bwana anaeleza:

**Jozi Na. 13**

**LC:** *They were going to the Atlantic – Caprice.* (pg. 42).

**LL:** "Walikuwa wanakwenda Atlantic – Caprice. (uk. 44).

Kupitia Data ya Jozi Na. 13, tunaona namna mandhari ya hoteli ya Atlantic – Caprice ilivyotafsiriwa. Mandhari hii imebeba maana ya kiishara inayoashiria matabaka katika jamii. Tunaona kuwa, katika jamii, kuna watu wenye uwezo au matajiri wanaoweza kumudu kuingia katika sehemu za starehe zenye kutumia gharama kubwa kama ilivyo katika hoteli ya Atlantic – Caprice. Shivji (2002) anaeleza kuwa kutokana na watu wachache kuhodhi rasilimali za nchi, kumekuwapo

na matabaka mawili, yaani wenye nacho na wasio nacho. Mandhari hii inasawiri uhalisi wa sehemu nyingi. Kwa mfano, hapa Tanzania, kuna baadhi ya hoteli ambazo ni za gharama kubwa kiasi kwamba mtu mwenye uwezo wa kawaida au wa chini hawezi kumudu kwenda kupata huduma.

Mandhari ya pili ni choo cha nyumbani kwa Yule Bwana. Mandharia hii imesawiriwa kwa kutumia lugha ya ishara. Mandhari ya choo inaelezwa kuanzia pale Koomson na mke wake Estella walipotembelea nyumbani kwa Yule Bwana. Ilifika wakati ambapo Koomson alibanwa na haja na kutaka kwenda chooni. Anaandika:

**Jozi Na. 14**

**LC**: *Nature is calling. Please take me to your toilet* (pg. 133).

**LL**: Nataka kwenda haja. Tafadhali nipeleke chooni (uk. 144).

Koomson anamwambia Yule Bwana ampeleke chooni kwa sababu alikuwa amebanwa na haja, ndipo Oyo ambaye ni mke wa Yule Bwana anajibu:

**Jozi Na. 15**

**LC:** "*We don't have a toilet here." Oyo looked astonished. Preening herself, Estella asked, 'So how do you er…what do you do?' The man, enjoying himself now, gave her a long reply. 'We have a place all right,' he said, 'only it isn't anything high class. It isn't a toilet, you see. Just a latrine*' (pgs. 133,134).

**LL:** "Hatuna choo hapa," Oyo akaonesha kushangaa. Estella akauliza, "Kwa hivyo nyinyi hu…hufanyaje? Yule bwana, huku anaona raha, akampa Estella kipande cha jawabu. "Choo kipo", akasema, lakini si cha kwendewa na watu wakubwa. Si choo kamili. Ni cha kunyia tu" (uk. 144).

Katika Data ya Jozi Na. 15, tunaona kuwa Oyo anasema kuwa wao hawana choo kwa sababu kilichopo si kizuri na ndiyo maana hapendelei kukiita choo badala yake anasema kuwa hicho ni cha kunyia tu. Utafiti umebaini kuwa mandhari hii ya choo cha Yule bwana inaashiria umasikini na hali duni ya maisha wanayoishi familia ya Yule bwana kwa kuwa wameshindwa kujenga choo kizuri.

Mandhari ya tatu ni choo cha ofisini kwa Yule bwana. Katika ML, mandhari hii imeelezwa kwa kutumia lugha ya ishara. Tunaona choo hiki kimesawiriwa katika mandhari yenye uchafu wa kila namna. Inaonekana watu wanatumia vyoo hivyo na kupaka mavi yao katika kuta za choo. Hii inaonekana pale inapoandikwa:

**Jozi Na. 16**

**LC**: *There must have been people who did not just forget to bring their paper, but who also did bother to drop their loads, for the wall has marks that are not mere after pieces, but large chunks of various shit* (pg. 106).

**LL**: Lazima kulikuwa na watu ambao si kwamba walisahau kuja na karatasi za kujifuta tu bali ambao hawakujali kamwe kuyafutia mavi yao kwenye kuta kwani kulikuwako na vidonge vinene vinene vya mavi (uk. 113).

Katika Data ya Jozi Na. 16, tunaona namna watu wanavyochafua choo kwa kupaka vinyesi vyao ukutani. Pia, waliandika maneno pamoja na michoro kwenye kuta za choo kama ifuatavyo:

**Jozi Na. 17**

**LC**: *A small drawing of sex in an impossible Indian position, with the careful lettering*: *VAGINA SWEET* (pg. 106).

**LL**: Picha yenyewe iliyochorwa ni ya mume na mke wafanyao kitendo kwa kutumia mtindo wa Kihindi usiowezekana. Chini yake kumeandikwa kwa hati nzuri: UCHI NI MTAMU (uk. 113).

Data ya Jozi Na. 17 inaonesha kuwa mandhari ya choo imechorwa picha ya mume na mke wakifanya mapenzi na kuandika matusi chini yake "uchi ni mtamu". John (2018) anasema kuwa katika utamaduni wa Waswahili, ni jambo lisilokubalika kutaja ama kuandika kwa namna ya uwazi sehemu za siri za binadamu. Mfasiri ametafsiri neno "vagina" kuwa ni "uchi" kwa namna ya kupunguza ukali wa maneno. Katika data ya Jozi Na. 17, inaonekana choo ni kichafu kutokana na kupakwa kinyesi na kuchorwa picha mbaya. Utafiti umebaini kuwa mandhari hii ya choo inayosawiriwa kwa kuandikwa kwa lugha ya matusi inawakilisha mambo mbalimbali. Mosi, katika utamaduni wa Kiafrika si jambo jema kutamka ama kuandika hadharani lugha ya matusi bila kutumia tafsida. Tunaona choo hicho kikiwa na lugha kali yenye kukera, kitu ambacho kinawakilisha kukosekana kwa maadili katika jamii. Pili, kitendo hiki kinabeba dhana ya uovu unaowahusu viongozi. Vyoo vinapatikana katika ofisi za umma lakini zimesheheni lugha ya matusi yenye kuashiria kuwa viongozi si waadilifu, mathalani, kupitia suala la rushwa ambalo limekuwa likishamiri katika jamii.

Mandhari ya nne ni mtaa wa Makao ya juu ambao anakaa Koomson na familia yake pamoja na familia zingine za watu wenye uwezo au matajiri. Mtaa huu unaonekana pale ambapo Yule Bwana na mkewe Oyo wanapokwenda kuwatembelea akina Koomson. Wakiwa njiani, Oyo anasema:

**Jozi Na. 18**

**LC**: *UPPER RESIDENTIAL AREA 'Go to the upper Residential Area, driver' said Oyo* (pg. 140).

**LL**: "Dereva, tunakwenda sehemu ya Makao ya Juu" Oyo akamwambia (uk. 152).

Data hii inaonesha majibizano kati ya Oyo na dereva wakiwa njiani kwenda kwa Koomson. Dereva hakujua maana ya ule mtaa; naye anauliza:

**Jozi Na. 19**

**LC**: '*And what does it mean at all, the name?' he asked. 'What name? asked the man. 'The name of this place,' said the driver, laughing* and *adding, 'I have never been able to pronounce it properly. I didn't stay long in school, you know'. 'Oh, the Residential Area?' 'Yes'. The man turned the name over in his mind, thinking of an explanation that would not sound too foolish. 'It means a place where people live'*. (pgs. 142, 143).

**LL**: "Ni nini maana ya jina hili?" Akauliza dereva. "Jina lipi?" Yule bwana akamuuliza. "Jina la mahali hapa", dereva akajibu, akacheka na akaendelea kusema, "siwezi kulitamka sawasawa. Sikusoma sana shule". "Ah, jina la mahali hapa?" "Ndiyo". Yule Bwana akawa analizungusha hilo jina ubongoni mwake na huku akifikiria maana ya kutoa na ambayo haitakuwa ya kijinga sana. "Maana yake ni mahali wanapoishi watu" (uk. 155).

Kupitia Data ya Jozi Na. 19, tunaona Yule Bwana anajaribu kujibu swali kuhusu maana ya jina la mtaa wa makao ya juu. Yule Bwana naye anaonekana kutojua maana halisi ya jina hilo, ndipo anasema ni mahali wanapoishi watu. Utafiti umebaini kuwa, mandhari hii imetumia lugha ya ishara ambayo inaleta maana tatu zifuatazo: Mosi, tunaona mandhari hii inadhihirisha matabaka yaliyopo katika jamii. Watu walio na uwezo wana mitaa yao wanayoishi. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba hali hii ipo hata Tanzania, mathalani, katika Jiji la Dar es Salaam kuna mitaa kama vile Oysterbay na Masaki ambayo wanaishi watu wenye uwezo. Pia, kuna mitaa mingine wanayoishi watu wenye hali ya kawaida kiuchumi kama vile Mbagala, Manzese na Tandale kwa kutaja michache. Pili, kupitia mandhari hii, tunaona kuna lugha ya ishara inayowakilisha ujinga walionao watu. Hapa tunaona dereva wa teksi pamoja na Yule Bwana hawaelewi vizuri maana halisi ya jina la

mtaa wa Makao ya juu. Tatu, suala lingine linaloibuka kutokana na mandhari hii, ni hali ya kujikweza (ujivuni) na madaha anayoonesha Oyo kwa dereva wa teksi kuwa anaufahamu sana mtaa wa makao ya juu kama kwamba ndiko anakoishi yeye ili aonekane yuko bora kuzidi dereva huyo.

Mandhari ya tano ni nyumba ya msimamizi wa mashua. Nyumba hii imesawiriwa kwa namna inayotumia lugha ya ishara. Hii imeonekana pale ambapo Yule Bwana anampeleka Koomson kuomba msaada kwa msimamizi wa mashua. Mwandishi anaeleza:

**Jozi Na. 20**

**LC**: *The two men entered. Finding nothing to sit on, they stood in the middle of the little room, the boatman facing them. On the floor at his feet there was his mat, laid out for sleeping on. A chopbox made out of the pale wood of packing cases stood against the back wall* (pg. 173).

**LL**: Wakaingia. Kwa vile hawakukiona kiti cha kukalia, wakabaki wamesimama katikati ya chumba kidogo na huyo mwenyeji wao amewaelekea. Chini kulikuwa na mkeka wake uliotandikwa ili kulalia kisanduku kilichotengenezwa kwa mbao zilizopauka na kilichokuwa kimeegemezwa kwenye ukuta ulioko nyuma (uk. 189).

Tukirejelea Data ya Jozi Na. 20, tunaona namna mandhari ya nyumba ya msimamizi wa mashua yalivyokuwa duni kiasi kwamba hapakuwa na viti vya kukalia. Tunaona Koomson na Yule bwana wanakaribishwa kukaa kwenye mkeka na kisanduku kilichotengenezwa kwa mbao zilizopauka. Utafiti umebaini kuwa hali hii inawakilisha umasikini ulioko kwenye nchi za ulimwengu wa tatu kama vile Ghana, Tanzania, Uganda na Kenya pamoja na nchi nyinginezo.

## 6.0 Hitimisho

Makala hii imejadili tafsiri ya lugha ya ishara katika riwaya ya *Wema Hawajazaliwa* kwa kujikita katika mtazamo wa kiulinganifu. Makala imejadili namna mfasiri wa *Wema Hawajazaliwa* alivyozingatia misingi ya ulinganifu wa kimawasiliano katika kuleta athari sawa kwa wasomaji wa matini lengwa kama ilivyo kwa wasomaji wa matini chanzi. Mfasiri kupitia vipengele vya matumizi ya wahusika wa kiishara, matukio ya kiishara na kichwa cha riwaya ameweza kutafsiri lugha ya ishara katika hali ya kuzingatia ulinganifu wa kimawasiliano. Aidha, makala inapendekeza wafasiri wa matini za kifasihi kuweka msisitizo katika kuzingatia ulinganifu wa kimawasiliano wanapotafsiri lugha ya ishara ili kuepusha upotoshaji wa ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa matini chanzi.

**Marejeleo**

Armah, A.K. (1969). *The Beautyful Ones are not Yet Born*. Johannesburg: Heinemann Publishers.

_____ (1969). *Wema Hawajazaliwa*. Mfasiri A. Abdallah. Nairobi: East African Educational Publishers Limited.

BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.

Catford, J. (1965. *A Linguistic Theory of Translation*. London: Oxford University Press.

Jilala, H. (2016). "Uchambuzi wa Nadharia ya Ulinganifu katika Fasihi". Katika H. Jilala (Mh.), *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Limited. Kur. 222 - 245.

John, B.N. (2018). *Usawiri wa Utamaduni wa Hadhira Lengwa katika Riwaya Zilizotafsiriwa kwa Kiswahili: Mifano kutoka Barua Ndefu kama Hii*. Tasinifu ya Umahiri (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kahigi, K. (1995). "Lugha katika Vitabu vya Watoto." *Kioo cha Lugha*. 1: 21-36.

Legere, A. (2009). *Origins of African Names*. London: Chapman and Hall Ltd.

Makaryk, I.R. (1993). *Enclopedia of Contemporary Literary Theory*: *Approaches*, *Scholars*, *Terms*. Canada: Toronto University Press.

Malangwa, P. (2005). *Problems of Translating Literary Works: The Case of Julius Kambarage Nyerere's Translation of the Play Mabepari wa Venisi*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nida, E. na Taber, C.R. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Shanghai: Foreign Language Education Press.

Nida, E. (1964). *Toward a Science of Translation*. Leiden: E. J. Brill.

Nida, E. na Taber, C.R. (1969. *The Theory and Practice of Translation*. Shanghai: Foreign Language Education Press.

Pembe, H. (2016). "Tafsiri ya Mazungumzo katika Filamu za Kiswahili". *Huria Journal of the Open University of Tanzania*. 21: 25- 40.

Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Reiss, K. (1971/ 2000). "Moglichketeiten und Grenzen der Ubersetzungskrititik, Munich: M. Hubeber", imetafsiriwa na E.F. Rhodes (2000), kama *Translation Criticism: Potential and Limitations*. Manchester: St. Jerome and American Bible Society.

Said, E. (1977). *Culture and Imperialism*. New York: Vintage Publishers.

Samweli, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Meveli Publishers.

Thomas, E. (2018). "Uzingativu wa Vipengele vya Kifani katika Kazi za Fasihi ya Kiswahili zilizotafsiriwa: Mifano kutoka Tamthilia ya *Julius Caezar"*. Katika Omari, S. na Samwel, M. (Wah.), *Fasihi*, *Lugha na Utamaduni wa Kiafrika*. Dar es Salaam: TUKI. Kur. 578 - 606.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi*: *Misingi ya Uchanganuzi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Wanyonyi, M.C. (2015). "Ishara na Uashiriaji kama Nyenzo ya Mtindo, Maana na Kiwakilishi cha Itikadi katika Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke"*. *Swahili Forum.* 22: 104 - 118.